**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**
**HALMASHAURI YA MANISPAA YA KIGAMBONI**
**SHULE YA SEKONDARI KIDETE**

**S.L.P 36078 KIGAMBONI** **DAR ES SALAAM**

Kumb: Na. KMC/KDTSS/US14/2020 Tarehe: ……………

Jina la Mwanafunzi: ____________________________

**YAH: MAELEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KIDETE WILAYA YA KIGAMBONI, MKOA WA DAR ES SALAAM, MWAKA 2020.**

**1.0. UTANGULIZI.**

Ninafurahi kukuharifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika Shule hii mwaka 20…. Hongera sana.

Shule ipo katika kata Mji mwema, Wilaya ya Kigamboni, Mkoa wa Dar es Salaam.

Muhula wa kuanza masomo unaanza tarehe …………….. unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe ……………. na mwisho wa kuripoti ni tarehe ……………. ndani ya siku saba, ukichelewa nafasi yako itajazwa na mtu mwingine.

**2.0. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA:-**

**2.1. SARE ZA SHULE**

Sare za shule itakuwa kama ifuatavyo:-

**A. WAVULANA**

- Suruali mbili rangi ya kijivu iliyoiva
- Mashati mawili meupe mikono mifupi
- Soksi jozi (pair) mbili nyeusi
- Mkanda mweusi
- Viatu vyeusi vya kamba vya ngozi
- Begi moja jeusi kwa ajili ya kubebea daftari na vitabu

**NB: Mshono usiwe wa kubana (MODAL)**

**B. WASICHANA**

- Sketi mbili rangi ya kijivu iliyoiva, mshono linda moja (box) kwa mbele na malinda mawili madogo pembeni. Sketi ni lazima ivuke magoti.
- Mashati mawili meupe mikono mifupi
- Soksi jozi (pair) mbili nyeupe
- Viatu vyeusi vya kamba vya ngozi
- Usukaji wa nywele ni wa mistari/matuta 5 – 7
- 

Scanned with CamScanner

**C. HIJAB**

- Sketi mbili rangi ya kijivu, mshono uwe hadi kwenye kisigino
- Blauzi mbili nyeupe (nusu kanzu) mikono mirefu
- Vitambaa viwili virefu visivyo na urembo
- Soksi jozi (pair) mbili nyeupe
- Viatu vyeusi vya kamba vya ngozi
- Begi moja jeusi kwa ajili ya kubebea daftari na vitabu.

**2.2. DARASANI**

i) Madaftari yasiyopungua 10 ukubwa wa kati (Counter book quire 2)
ii) Mkebe wa vifaa vya Hisabati (Mathematical Set).
iii) Peni, rula, kifutio na penseli
iv) Office file kwa ajili ya kuwekea kumbukumbu za mwanafunzi
v) Oxford English Dictionary

**3.0. USAFI NA E/K**

i) Mwanafunzi aje na kifaa kimojawapo kati ya Jembe lenye mpini, Fyekeo (Slasher) na fagio wa ndani na nje.

**4.0. USAJILI**

4.1. a) Unatakiwa kuchukua fomu maalum kwa ajili ya uchunguzi wa afya yako (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Daktari wa Hospitali ya Serikali tu, na utarejesha kwa Mkuu wa Shule.

b) Utajaza fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya Mwanafunzi, mkataba wa utiifu, kutoshiriki migomo, fujo na makosa ya jinai.

c) Mzazi pia atajaza fomu ya kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelezo mengine yatakayotolewa na shule.

- **Unatakiwa kusoma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.**

**NAKUKARIBISHA SANA KATIKA SHULE HII**

..........................

**HALIFA YONGO**
**MKUU WA SHULE**
**0783 592291/0713 016266**

Scanned with CamScanner

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAISI**
**WIZARA YA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA MANISPAA YA KIGAMBONI**

---

# SHULE YA SEKONDARI KIDETE

## SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

1. Kila mwanafunzi anawajibika kuwaheshimu viongozi wa shule, walimu, wafanyakazi, wasio walimu, wanajumuiya wanaoizunguka shule, wazazi/walezi, na wanafunzi wenzake.
2. Kila mwanafunzi analazimika kuhudhuria katika shughuli zote za kitaaluma ndani na nje ya shule.
3. Kila mwanafunzi anatakiwa kufanya kazi zote za shule anazopewa na uongozi wa shule, walimu, walimu wa masomo, na viongozi wa serikali ya wanafunzi kwa usahihi na umakini.
4. Kila mwanafunzi anatakiwa kuwahi katika kila shughuli za shule ikiwa ni pamoja na kuwahi shuleni na kuwepo shuleni wakati wote wa ratiba za shule.
5. Kila mwanafunzi anatakiwa kuifahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wake hapa shuleni.
6. Kila mwanafunzi anatakiwa kuwamsafi yeye binafsi, mavazi yake kuwa nadhifu, kuwa katika sare rasmi ya shule na pia kutunza mazingira ya shule.
7. Kila mwanafunzi anatakiwa kuzingatia ratiba ya shule wakati wote awapo shuleni.
8. Kila mwanafunzi anatakiwa kusalimia watu anaokutana nao iwe ndani au nje ya mipaka ya shule.
9. Makosa yanayoweza kusababisha mwanafunzi kufukuzwa shule ni:-
   a) Wizi.
   b) Uasherati.
   c) Ulevi, uchezaji kamari wa aina yoyote, matumizi ya bangi, milungi na madawa ya kulevya.
   d) Makosa yote ya jinai kwa mujibu wa sheria za nchi.
   e) Kupiga au kupigana

Scanned with CamScanner

f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.

g) Kudharau wimbo wa Taifa na Bendera ya Taifa.

h) Kuoa au kuolewa.

i) Kupata ujauzito (mimba) au kusababisha mimba ndani na nje ya mipaka ya shule na ikadhibitika bila ya kuacha shaka.

j) Kutoa mimba.

k) Kugoma, kuchochea au kuongoza migomo inayoweza kuvuruga amani na usalama wa shule na watu.

l) Kugomea adhabu halali.

m) Kukutwa vichakani kabla, baada au wakati wa masomo, ikiwa ni pamoja na kukutwa maeneo ya Beach wakati wa masomo.

10. Vitu visvyoruhusiwa shuleni:-

a. Kuvaa pete, mikufu,cheni, hereni, culture, na bangili.
b. Kuvaa milegezo (kata–k), models, mashati ya kubana, sketi fupi, nikabu.
c. Kunyoa nyusi, vipara, kupaka kucha rangi, hina, kujichora michoro mwilini (tattoos).
d. Kufuga kucha ndefu, ndevu au nywele nyingi.
e. Kusuka mitindo, kukali, ku-relax nywele, na kupaka dawa nywele.

   NB: Wasichana wanatakiwa kusuka nywele zao kwa kwenda nyuma mistari kati ya tano na saba.
f. Kuvaa kandambili, katambuga, raba, mabuti, bajaji, sandals na viatu vingine vyovyote ambavyo siyo sare rasmi ya shule, kuvaa mikanda yenye vyuma vikubwa.
g. Simu za mkononi haziruhusiwi shuleni.
h. Kila mwanafunzi anatakiwa kutumia usafiri rasmi kuja shuleni na kurudi nyumbani, hairuhusiwi kukaa barabarani kuomba lifti kwa watu usiowajua au kudandia magari ya mchanga na kokoto.

- **MUHIMU**

KILA MWANAFUNZI ANATAKIWA KUZISOMA, KUZIELEWA NA KUZITEKELEZA SHERIA NA KANUNI HIZO HAPO JUU.

*"KIDETE YENYE KUTOA ELIMU ILIYO BORA INAWEZEKANA, KILA MMOJA ATIMIZE WAJIBU WAKE"*

IMETOLEWA NA MKUU WA SHULE.

Scanned with CamScanner

OFISI YA RAIS – TAMISEMI
HALMASHAURI YA MANISPAA YA KIGAMBONI
SHULE YA SEKONDARI KIDETE

S.L.P 36078 KIGAMBONI DAR ES SALAAM

## FOMU YA KUANDIKISHWA

### A. IJAZWE NA MWANAFUNZI

1. Jina la Mwanafunzi: ____________________
2. Taifa: ____________________
3. Uraia: ____________________
4. Dini: ____________________
5. Tarehe ya kuzaliwa: ____________________
6. Shule ya msingi aliyotoka: ____________________
7. Mwaka wa kumaliza shule hiyo: ____________________

**Saini ya Mwanafunzi:** ____________________ **Tarehe** ____________

### B. MAELEZO BINAFSI YA MZAZI/MLEZI

1. Jina kamili la Mzazi/Mlezi: ____________________
2. Taifa: ____________________
3. Uraia: ____________________
4. Anuani kamili mjini Dar es Salaam: ____________________
5. Sehemu anayoishi: ____________________
6. Mtaa: ____________________
7. Simu ya mkononi: ______________ Ofisini: ______________

### C. MAELEZO YA KIKAZI YA MZAZI/MLEZI

- Jina la Mwajiri: ____________________
- Anuani yake: ____________________
- Kazi ya Mzazi/Mlezi (Meneja, Karani, Daktari, Mfanya biashara n.k.) ____________________

### D. SOMO LA DINI

Mimi ______________________________ ambae ni Mzazi /Mlezi ______________________________ ninamruhusu mtoto wangu kuhudhuria somo la dini ya ______________ Dhehebu ______________ siku ya kipindi cha Dini akiwa shuleni Kidete Sekondari.

**Sahihi ya Mzazi/Mlezi** ____________________ **Tarehe** ____________

Scanned with CamScanner

KIAMBATANISHO 'C'

# THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
# KIDETE SECONDARY SCHOOL

## REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

To be filled by the Government Medical Officer and return to the HEAD OF KIDETE SECONDARY SCHOOL, P. O. BOX 36078 Dar es salaam.

To the medical

.........................................

.........................................

.........................................

A: RE: ..........................................................................................

Please examine the above mentioned student and comment on his/her fitness by responding to the problems below Say Yes or No to each problem and if Yes then state.

HEADMASTER DATE.........................................

Insert (✓) in the boxes provided

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI KIDETE
P.O. Box 36078
MJIMWEMA-KIGAMBONI
DAR-ES-SALAAM

| | | | |
|---|---|---|---|
| i. | Hearing | Yes [ ] | No [ ] |
| ii. | Speech | Yes [ ] | No [ ] |
| iii. | Sight | Yes [ ] | No [ ] |
| iv. | T.5 | Yes [ ] | No [ ] |
| v. | B.P. | Yes [ ] | No [ ] |
| vi. | Diabetes | Yes [ ] | No [ ] |
| vii. | Mental case | Yes [ ] | No [ ] |
| viii. | Physical disability | Yes [ ] | No [ ] |

ix. Any other ..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

B. Recommend if the student is fit for studentship (i) YES or NO

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

C. Any other advice ......................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

...............................

Name and signature ............................................ Time ...............................

Date...............................

Scanned with CamScanner